
# PROGRAMA CISTERNAS

**PROGRAMU YA KITAIFA YA KUSAIDIA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA NA TEKNOLOJIA NYINGINE ZA KIJAMII KWA UPATIKANAJI WA MAJI**



GLOBAL ALLIANCE AGAINST HUNGER AND POVERTY

WIZARA YA MAENOELEONA MSAADA WA KIJAMII,FAMILIA NAKUPAMBANA NA NJAA

SERIKALI YA BRASIL
UPANDE WA WATU WA BRAZILI

## Maelezo ya kiufundi

**José Wellington Barroso de Araújo Dias**
Waziri wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii, Familia na Mapambano dhidi ya Njaa

**Lilian dos Santos Rahal**
Katibu wa Kitaifaya Usalama wa Chakula na Lishe

**Adriana Telles Ribeiro**
Mkuu wa Kitengo Maalum cha Ushauri wa Masuala ya Kimataifa

**Camile Marques Sahb**
Mkurugenzi wa Idara ya Kukuza Ujumuishaji Wenye Tija Vijijini na Upatikanaji wa Maji

**Vitor Leal Santana**
Mratibu Mkuu wa Upatikanaji wa Maji

**Clarita Rickli**
Meneja wa Mradi wa Mawasiliano katika Sekretarieti ya Kitaifa ya Usalama wa Chakula na Lishe

**Mpango wa Matangi ya Maji**
Alisson Martins Ramos
Ândrea Colares
Carolina Tavares da Silva Bernardo
Cleyton Domingues de Moura
Domiciano Ferreira Gomes Filho
Erica Veruska de Sena Lima Pereira
Everton Aparecido da Costa
Glicério Siqueira Silva de Barros
Henrique Silva Petrocell
Marta Rodrigues Leite
Myriam Cyntia Cesar de Oliveira
Patrícia Laundry Mollo Vieira
Rivia Ryker Bandeira de Alencar
Roberta Pelella Mélega Cortizo
Valdenir Marinho Rosa
Victor Santos Moraes
Viviam Catarina de Oliveira
Yara da Silva Farias

**Ubunifu wa dhana na mpangilio wa kurasa**
ASCOM – MDS

**Tafsiri**
AESSIN – MDS

# PROGRAMU YA KITAIFA YA KUSAIDIA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA NA TEKNOLOJIA NYINGINE ZA KIJAMII KWA UPATIKANAJI WA MAJI

## MPANGO WA HODHI

# UTANGULIZI

Programu ya Kitaifa ya Kusaidia Uvunaji wa Maji ya Mvua na Teknolojia Nyingine za Kijamii za Upatikanaji wa Maji inatekelezwa na Serikali ya Shirikisho tangu mwaka 2003.

Ukijulikana kama Mpango wa Hodhi, lengo lake ni kuimarisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo na kwa ajili ya uzalishaji wa chakula kwa familia za vijijini zenye kipato cha chini na miundombinu ya umma ya vijijini - hasa shule - iliyoathiriwa na ukame au uhaba wa maji wa mara kwa mara.

Udhibiti wa sasa unazingatia Sheria Nambari 12,873 ya mwaka 2013, Agizo la Rais Nambari 9,606 la mwaka 2018, na seti ya kanuni nyingine za nyongeza.

Fungua ukurasa kupitia msimbo wa QR ili kufahamu zaidi kuhusu sheria na kanuni zilizopo.





Mpango wa Hodhi unatofautiana na sera zingine za umma za upatikanaji wa maji kwa kuunga mkono teknolojia za kijamii, ambazo zina sifa ya kuwa rahisi, za gharama nafuu, na rahisi kusimamiwa na kufanyiwa matengenezo na walengwa wenyewe. Zaidi ya hayo, katika utekelezaji wa teknolojia hizi, michakato ya uhamasishaji wa jamii na mafunzo kwa walengwa ni muhimu sawa na ujenzi wenyewe wa miundombinu ya ukusanyaji na uhifadhi wa maji. Kwa kuishirikisha jamii katika kila hatua ya mchakato, inatarajiwa kuimarisha uendelevu wa mafanikio ya kijamii yanayotokana na upatikanaji wa maji salama.

Mpango huu unatekelezwa kupitia ushirikiano kati ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii na serikali za mikoa na wilaya, muungano wa mamlaka za miji, pamoja na mashirika ya kiraia.

Katika miaka ya hivi karibuni, kipaumbele cha utekelezaji kimekuwa katika maeneo ya nusu-jangwa na Amazon, maeneo yenye sifa tofauti za hali ya hewa na mazingira, lakini ambapo idadi ya watu wa vijijini wanaoishi katika umaskini wanakabiliwa na changamoto za kupata maji safi; ama kwa sababu ya uhaba wa wingi na ubora, kama ilivyo katika eneo la kwanza, au kimsingi kwa sababu ya ukosefu wa maji ya kunywa, kama ilivyo katika eneo la pili. Pamoja na hayo, **Mpango huu unahusisha nchi nzima na unalenga kutatua changamoto za maji kwa kutumia teknolojia zilizolingana na muktadha wa kila eneo, utamaduni na jamii.**



# AINA ZA TEKNOLOJIA ZA KIJAMII KATIKA MPANGO WA MATANGI






## Tangi ya Sahani ya Lita 16,000

Ni tangi la matofali la lita 16,000 lililounganishwa na mfumo wa mifereji ya maji iliyowekwa kwenye paa la nyumba ili kukusanya maji ya mvua. Uwezo wake wa kuhifadhi maji ulibuniwa ili kukidhi mahitaji ya haraka ya maji ya familia inayoishi katika eneo hili lenye ukame, kwa ajili ya kunywa na kupika.



## Tangi ya Shule ya Lita 52,000

Inajumuisha tangi iliyojengwa kwa sahani za uashi yenye uwezo wa kuhifadhi hadi lita 52,000 za maji, ambayo imeunganishwa na paa la shule. Tangi hii imekadiriawa kutosheleza mahitaji ya maji ya jamii ya shule, ikijumuisha maji ya kunywa na ukulima wa bustani, kulingana na idadi ya wanafunzi na ukubwa wa shule.





## Tangi ya Sakafu ya Lita 52,000

Inajumuisha tangi iliyojengwa kwa sahani za uashi yenye uwezo wa kuhifadhi hadi lita 52,000 za maji, ambayo imeunganishwa na eneo la kuvunia maji lenye ukubwa wa mita za mraba 200. Eneo hili limetengwa kwa ukingo na liko kwenye sehemu ya juu kuliko ilipo hodhi hiyo. Teknolojia hii imekadiriwa kutosheleza mahitaji ya familia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na ufugaji wa wanyama wadogo.





## Tangi ya Maji ya Mtiririko ya Lita 52,000

Inajumuisha tangi iliyojengwa kwa sahani za uashi yenye uwezo wa kuhifadhi hadi lita 52,000 za maji, iliyounganishwa na eneo linalokusanya maji ya mtiririko ardhini. Teknolojia hii imekadiriwa kutosheleza mahitaji ya familia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na ufugaji wa wanyama wadogo.






## Tangi ya Paa Kubwa ya Matumizi Mbalimbali

Inajumuisha tangi iliyojengwa kwa sahani za uashi yenye uwezo wa kuhifadhi hadi lita 25,000 za maji, iliyounganishwa na banda lenye ukubwa wa mita za mraba 40 au 80, lenye paa kwa ajili ya kuvunia maji ya mvua. Teknolojia hii imekadiriwa kutosheleza mahitaji ya maji ya familia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na/au uzalishaji wa chakula na ufugaji wa wanyama wadogo.





## Bwawa la Chini ya Ardhi

Inajumuisha kizuizi kilichojengwa kukatiza mkondo wa maji ya mtiririko, vijito, au mito ya msimu, kwa kuweka nailoni imara kwenye mfereji uliochimbiwa hadi kufikia tabaka la ardhi lisilopitisha maji. Kazi yake ni kuhifadhi maji ndani ya udongo, jambo linalosababisha kutokea au kupanda kwa kiwango cha maji chini ya ardhi. Teknolojia hii imekadiriwa kutosheleza mahitaji ya familia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na ufugaji wa wanyama wadogo.



## Bwawa la Mfereji

Teknolojia hii inajumuisha bwawa lililochimbwa ardhini hadi kufikia tabaka lisilopitisha maji, likiwa na kuta za wima ambazo ni nyembamba na zenye kina kirefu, likiwa na uwezo wa kuhifadhi angalau lita 500,000 za maji. Teknolojia hii imekadiriwa kutosheleza mahitaji ya familia kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na, hasa, ufugaji wa wanyama.









## Mfumo wa kutibu na kutumia tena maji ya nyumbani

Teknolojia hii inajumuisha mfumo wa kuunganisha mabomba ya maji, sanduku la kunasa mafuta, kifaa cha kuchuja, tangi la kuhifadhia maji ya kutumiwa tena, na tangi la mvuke (kwa mfumo unaotumia choo cha ikolojia), tangi la maji, pamoja na pembejeo na vifaa vya kuendeleza mradi wa uzalishaji. Kuna aina mbili za teknolojia hii: 1) mfumo unaotibu na kutumia tena maji ya nyumbani pekee; na 2) mfumo unaotibu na kutumia tena maji taka yote ya nyumbani, ikiwa ni pamoja na choo cha ikolojia.






## Mfumo wa kijamii wa matumizi mengi ya maji ya mvua

Teknolojia hii inajumuisha: I) sehemu ya nyumbani yenye mfumo wa kuvuna maji ya mvua kutoka kwenye paa, tangi la juu la lita 1,000, choo na bafu la ndani (lenye mshunzi, beseni, na choo cha kukaa), na shimo la kupotezea maji taka; na II) sehemu ya kijamii ya kusambaza maji inayotumika wakati wa uhaba wa mvua, ikijumuisha uvunaji wa maji kutoka vyanzo mbadala (mito, chemchemi au visima), mfumo wa kusafisha maji kwa kichungi cha mchanga, na mtandao wa kusambaza maji kwa kila familia. Teknolojia hii ina mifumo tofauti kulingana na mazingira ya kando ya mto au nchi kavu.





## Mfumo wa kijitegemea wa matumizi mengi ya maji ya mvua

Inajumuisha mfumo wa nyumbani wa kuvuna maji ya mvua kutoka kwenye paa, tangi la juu la lita 1,000, tangi la ziada la lita 5,000, choo na bafu la ndani (lenye mshunzi, beseni na choo cha kukaa), na shimo la kupotezea maji taka.



## Mfumo mdogo wa usambazaji maji wenye vituo vya kijamii

Teknolojia hii inajumuisha miundombinu ya kuvuna maji kutoka juu ya ardhi, yakisukumwa na pampu inayotumia nishati ya jua, mtambo rahisi wa kusafisha maji kwa kutumia kichungi cha mchanga, Matangi ya kuhifadhia maji yaliyosafishwa na mtandao wa mabomba unaosambaza maji hayo hadi kwenye vituo vya pamoja vya kuchotea.





# MBINU ZA UTEKELEZAJI WA TEKNOLOJIA ZA KIJAMII

Utekelezaji wa teknolojia za kijamii katika Mpango wa Hodhi unajumuisha shughuli za uhamasishaji wa jamii, mafunzo kwa walengwa kuhusu usimamizi wa maji, na ujenzi au ufungaji wa miundombinu ya kuvuna na kuhifadhi maji.

**Uhamasijaji wa kijamii na uteuzi**

- Mikutano au makongamano ya kijamii
- Kamati ya eneo

**Mchakato wa mafunzo**

- Usimamizi wa maji
- Kubadilishana uzoefu
- Mbinu za ujenzi

**Muundo wa ukusanyaji na uhifadhi wa maji**

- Vifaa vya ujenzi
- Nguvu kazi
- Vifaa vya ziada

**Ufuatiliaji wa familia kwa ujumuishaji wa uzalisiaji**

- Tathmini (uchunguzi)
- Uundaji wa mradi wa uzalisjaji
- Uf uatiliaji wa mtu binafsi na/au wa kilundi

* Shughuli inayopangwa tu kwa ajili ya teknolojia zinazojumuisha Huduma ya Ushauri kwa Familia kwa ajili ya Ujumuishi wa Kijamii na Uzalishaji (SAFISP).



# HATUA YA 1: Uhamasishaji na uteuzi wa walengwa

Mchakato wa uhamasishaji wa kijamii na uteuzi wa walengwa unapaswa kufanyika kwa njia ya ushirikiano, ukihusisha wawakilishi wa serikali na mashirika ya kijamii - wakikusanyika kama kamati ya manispaa, ambao wana jukumu la kuamua vijiji vitakavyopata huduma.

## Vigezo vya uteuzi

Ili kushiriki katika Programu hii, familia lazima ziwe zimesajiliwa katika Daftari la Kitaifa la Programu za Kijamii za Serikali ya Shirikisho, ziwe na kipato cha chini ya nusu ya mshahara wa chini kabisa kwa kila mtu, ziwe zinaishi maeneo ya vijijini na zisiwe na vyanzo salama na vya kudumu vya kupata maji. Shirika linalotekeleza mradi litalazimika kuteua familia kulingana na vigezo vifuatavyo vya kipaumbele:

- **i** Familia zenye sifa za kupata msaada wa Bolsa Família, zikiwa na kipato cha kila mwezi kisichozidi R$ 218.00 (Reais mia mbili na kumi na nane) kwa kila mtu, kinachojulikana kama mstari wa umaskini;
- **ii** Familia kutoka kwa jamii za kitamaduni au watu wa kiasili;
- **iii** Familia zinazoongozwa na wanawake;
- **iv** Familia zenye idadi kubwa ya watoto wenye umri wa kuanzia miaka 0 hadi 6;
- **v** Familia zenye idadi kubwa ya watoto na vijana walio katika umri wa kwenda shule; na
- **vi** Familia zenye watu wanaoishi na ulemavu.

Kwa upande wa shule, zitakazopata msaada ni zile zilizopo maeneo ya vijijini, za serikali, na ambazo hazina ufikiaji wa mfumo wa maji wa umma au chanzo kingine chochote cha kudumu na salama cha maji.

# HATUA YA 2: Michakato ya Mafunzo

Mara tu familia zinapochaguliwa katika mchakato wa uhamasishaji wa jamii, ni lazima zishiriki katika shughuli za mafunzo. Hatua hii ya uwezeshaji ni muhimu sana, kwani ndipo maelekezo kuhusu usimamizi na matumizi ya maji yanapotolewa, pamoja na taratibu za matengenezo ya teknolojia husika

Zaidi ya hayo, pia kuna mipango ya mafunzo ya ujenzi wa teknolojia hizi. Lengo la hatua hii ni kuwahusisha walengwa moja kwa moja katika mchakato wa ujenzi.

Mchakato huu wa kielimu unatekeleza jukumu lingine la msingi katika mfumo wa teknolojia za kijamii, ambalo ni kubadilishana uzoefu na maarifa kuhusu mabadiliko na mwingiliano na mazingira pamoja na hali ya hewa ambamo familia husika zimejikita. Tarajio la shughuli hizi za mafunzo ni kupanua uelewa wa walengwa kuhusu mapungufu na uwezo wa teknolojia hiyo, na kwa njia hiyo, kuhakikisha athari za kudumu ambazo zimeoanishwa na hali halisi za maeneo husika.

# Hatua ya 3: Mchakato wa Ujenzi

Haiwezekani kutabiri muda unaohitajika kwa ajili ya ujenzi (au usakinishaji) wa kila teknolojia, kwani hii inatofautiana kulingana na hali halisi ya kila eneo. Kwa sababu hiyo, kipaumbele katika hatua hii ni ununuzi wa vifaa na uteuzi wa nguvu kazi kutoka ndani ya eneo husika, kama njia ya kupunguza gharama na kutengeneza fursa za kazi, hivyo kuchochea uchumi wa ndani.

## Hatua ya 4: Huduma ya Usaidizi wa Familia kwa Ujumuishi wa Kijamii na Wenye Tija (SAFISP)

Baadhi ya teknolojia za kijamii pia hujumuisha katika shughuli zao huduma ya usaidizi wa familia kwa ajili ya ujumuishaji wa kijamii na uzalishaji (SAFISP), ambayo kwa sasa inadhibitiwa na Agizo la MDS Nambari 961 la Februari 19, 2024. Huduma hii inajumuisha utambuzi, uundaji wa mradi wenye tija na shughuli za usaidizi wa kibinafsi na wa pamoja wa familia.

Katika hali hii, inawezekana kuunganisha Mpango wa Matangi na Mpango wa Kukuza Shughuli za Uzalishaji Vijijini, kupitia utoaji wa rasilimali za kifedha zisizorejesheka ambazo, kwa sasa, jumla yake ni R$ 4,600.00 – zinazotolewa kwa mafungu mawili – kwa ajili ya kuendeleza miradi ya uzalishaji.

Ushirikiano kati ya msaada wa kiufundi na kifedha ni njia ya kuzisaidia familia ili ziweze kujiimarisha au kupanua uwezo wao wa uzalishaji, kwa lengo la kuongeza au kubadilisha aina za uzalishaji wa chakula na shughuli za kuingiza kipato, hivyo kuchangia katika kuboresha usalama wa chakula na lishe pamoja na kupambana na hali ya umaskini.







# MFUMO WA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa Mpango wa Matangi unafanyika kwa mfumo wa kurejesha madaraka kwa wananchi na unategemea ushirikiano na:

- **Mashirika au vyombo vya umma** kama vile serikali za majimbo na serikali za manispaa na muungano wa umma wa manispaa, wakati wa kusaini mikataba, kwa mujibu wa Amri Nambari 11531 ya 2023 na Amri ya Pamoja MGI/MF/CGU Nambari 33 ya 2023; au
- **Mashirika ya kiraia,** wakati wa kusaini mikataba ya ushirikiano au mikataba ya ufadhili, kwa mujibu wa masharti ya Sheria Nambari 13.019 ya 2014 na Amri Nambari 8.726 ya 2016.

Uteuzi wa washirika unaweza kufanyika kwa njia ya moja kwa moja, kupitia ilani ya maelezo ya sababu au msamaha wa uteuzi wa umma – kwa kuzingatia sheria iliyopo, au kupitia ilani ya wito wa umma.

Baada ya uteuzi wa washirika na kuridhia kwa hati mahususi, washirika wa MDS katika utekelezaji wa Mpango lazima wateue na kuajiri mashirika ya kiraia yasiyo ya kiserikali kupitia Ilani ya Wito wa Umma , ambapo ni mashirika yaliyoidhinishwa awali na MDS pekee yanayoweza kushiriki. Ikumbukwe kuwa mchakato wa upataji wa idhini kwa mashirika yanayofanya kazi kama watekelezaji wa Mpango wa Matangi kwa sasa unasimamiwa na Agizo Nambari 22 la mwaka 2020, ambalo huweka kanuni na vigezo kwa ajili hiyo.

Sawa na ilani ya wito wa umma, hata mkataba wenyewe wa utoaji wa huduma utakaotiwa saini na mashirika ya utekelezaji, ni nyaraka zenye mifumo iliyowekwa na MDS, kulingana na Agizo la MDS Nambari 992 la mwaka 2024 na marekebisho yake. Katika ilani ya wito wa umma na mkataba, ni lazima iainishwe shabaha kuu kwa kila fungu, aina za teknolojia zitakazotekelezwa na thamani ya rejea ya kila kitengo, kama ilivyoelezwa katika miongozo mahususi ya kisheria, pamoja na seti ya kanuni nyingine zinazopaswa kuzingatiwa na washirika na watekelezaji katika eneo husika.

Kanuni za Mpango wa Matangi zinatoa uwezekano wa utoaji wa rasilimali mapema kwa mashirika ya utekelezaji, kwa kiwango cha hadi 30% ya thamani ya jumla ya mkataba uliotiwa saini, kama njia ya kuwezesha kuanza rasmi kwa utekelezaji wa mradi.

Picha hapa chini [rekebisha mpangilio] inaonyesha hatua kwa hatua za mchakato wa utekelezaji wa Mpango, kuanzia kuridhia kwa ushirikiano hadi uwasilishaji wa ripoti ya kazi (prestação de contas física), ambao unafanywa kupitia mfumo wa SIG Cisternas.



WIZARA YA MAENDELEO NA MSAADA WA KIJAMII, FAMILIA NA KUPAMBANA NA NJAA

SERIKALI YA BRASIL
UPANDE WA WATU WA BRAZILI

Mkataba au Hati ya Ushirikiano/Ufadhili

Jimbo, manispaa, muungano wa manispaa
au mashirika ya asasi za kiraia

**Tangazo la wito wa umma**
Agizo la Wizara Na. 992/2024


Utoaji wa kandarasi bila zabuni
Agizo la Wizara Na. 992/2024
Sheria Na. 14.133/2021

Mashirika binafsi yasiyo ya faida, yaliyoidhinishwa na Wizara
Agizo la Wizara Na. 22/2020

**Malipo ya awali ya hadi 30%**
Sheria Na. 12.873/2013
Amri Na. 9.606/2018

Usajili wa utekelezaji na uwasilishaji wa hesabu katika mfumo wa kidijitali
(SIG Cisternas)

Hati ya kupokea teknolojia ya kijamii








# UDHIBITI WA KIJAMII, UWAZI NA USIMAMIZI

MDS imekuwa ikiendeleza na kuboresha seti ya nyaraka zinazowezesha udhibiti mkubwa wa kijamii na ambazo zinalenga kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya Mpango pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za umma zilizotengwa kwa ajili yake.

## KAMATI ZA MANISPAA ZINAZOWAKILISHA JAMII

Udhibiti wa kijamii wa Mpango huu unaanza tangu mwanzo wa mchakato wa uteuzi wa walengwa. Kwa ajili hiyo, katika ngazi ya mahali husika, huundwa kile kinachoitwa kamati za manispaa zinazowakilisha jamii, ambazo zinahusisha ushiriki wa viongozi wa jamii, wahudumu wa afya wa jamii, wanachama wa mabaraza ya ndani, na mamlaka ya umma ya eneo husika, ambao husaidia kutambua familia zinazokidhi vigezo vya Mpango. Aidha, kamati hizo husaidia, inapohitajika, katika kuweka kipaumbele kwa jamii na walengwa watakaohudumiwa.

## SIG CISTERNAS (MFUMO WA TAARIFA NA USIMAMIZI WA MPANGO WA MATANGI)

Mpango wa Matangi pia una mfumo wa kusajili na kufuatilia utekelezaji unaoitwa SIG Cisternas. Kupitia mfumo huu, inawezekana kufuatilia utekelezaji wa hati za ushirikiano zilizotiwa saini, ikiwa ni pamoja na hatua mbalimbali za utekelezaji wa teknolojia (uteuzi, mafunzo na utoaji wa teknolojia). Uwasilishaji wa ripoti za kazi kwa mikataba iliyotiwa saini kati ya mshirika wa MDS na shirika la utekelezaji unafanywa kupitia zana hii, ambapo taarifa kuhusu familia zilizochaguliwa, michakato ya mafunzo yaliyofanyika, na teknolojia zilizowekwa huingizwa.

Kwa kila teknolojia, ni lazima itolewe hati ya makabidhiano, iliyotiwa saini na walengwa, ikiwa na maelezo yanayowezesha kuitofautisha, kama vile jina kamili la mlengwa, jamii, tarehe ya kuanza na kukamilika kwa ujenzi, namba ya utambulisho, na picha za ushahidi. Aidha, kwa sasa teknolojia zote za kijamii zinazotekelezwa chini ya Mpango wa Matangi zina vielelezo vya kijiografia (GPS) vinavyowezesha utambuzi wa mahali zilipo kwa haraka.






# KANUNI KUU ZA MPANGO WA MATANGI

Kwas asa, Mpango wa Matangi una miongozo ya kisheria ifuatayo:

- Sheria Nambari 12,873 ya tarehe 24 Oktoba 2013. Inaanzisha Mpango wa Kitaifa wa Kusaidia Uvunaji wa Maji ya Mvua na Teknolojia Nyingine za Kijamii kwa ajili ya Upatikanaji wa Maji - Mpango wa Matangi.

- Amri Nambari 9,606 ya tarehe 10 Desemba 2018. Inatoa kanuni za Programu ya Kitaifa ya Kusaidia Uvunaji wa Maji ya Mvua na Teknolojia Nyingine za Kijamii kwa ajili ya Upatikanaji wa Maji - Mpango wa Matangi.

- Agizo la SESAN Nambari 213 la tarehe 26 Novemba 2025. Inaweka sheria na taratibu za kuidhinisha mashirika yasiyo ya kiserikali katika mfumo wa Mpango wa Matangi.

- Agizo la MDS Nambari 992 la tarehe 4 Juni 2024. Inafafanua hati za kisheria zinazopaswa kutumiwa na washirika wa MDS katika utekelezaji wa Mpango wa Matangi.

- Agizo la SESAN Nambari 168 la tarehe 1 Agosti 2025. Inaweka sheria na taratibu za kufuatwa kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji na udhibiti wa mikataba iliyosainiwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Matangi.

- Miongozo ya Kisheria. Nyaraka zinazobainisha gharama ya marejeleo ya kila kitengo na mbinu za utekelezaji wa teknolojia za kijamii za Mpango huu. Teknolojia zinazosaidiwa hivi sasa, pamoja na maelekezo ya utendaji yanayotumika sasa yanapatikana kwenye ukurasa ufuatao: https://www.gov.br/mds/pt-br/acoes-e-programas/acesso-a-alimentos-ea-agua/programa-cisternas/tecnologias-sociais.



# Mawasiliano kama sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Matangi

Mnamo Machi 2026, Amri Nambari 35 ilichapishwa, ikifafanua mawasiliano ya kijamii kama sehemu ya kimkakati katika utekelezaji wa Programu ya Matangi. Lengo la kanuni hiyo ni kuboresha michakato ya uhamasishaji wa jamii na walengwa, pamoja na kuhakikisha uwazi kwa umma kuhusu shughuli zinazotekelezwa.

Amri hiyo mpya inaonyesha mtazamo wa kuwaona watu kama raia wenye haki, ikiwa ni pamoja na haki ya binadamu ya kupata chakula cha kutosha, ambayo inajumuisha pia haki ya kupata maji salama.

**“Sio kwa kukaza fundo ndipo mtu anaponaswa.”**

Kama njia ya kurahisisha mchakato huu, kanuni mpya inautambua Mtandao wa Mawasiliano wa Programu ya Matangi kama chombo shirikishi, kilichoundwa ili kuratibu na kuongeza juhudi za mawasiliano kati ya Serikali ya Shirikisho, washirika, na vyombo vinavyotekeleza Programu ya Matangi, kupitia ushiriki wa wawakilishi wa maeneo yao husika ya mawasiliano.

Malengo ya Mtandao wa Mawasiliano wa Programu ya Matangi, kama yalivyoanzishwa na kanuni hiyo, ni:

- Kuimarisha mchakato wa utekelezaji wa Programu ya Matangi kwa walengwa;
- Kuhakikisha kwamba ujumbe kuhusu Haki ya Binadamu ya Kupata Chakula cha Kutosha unawafikia walengwa wa Programu na wadau wengine kwa njia iliyo wazi na inayozingatia muktadha. (Aya moja.)

Mtandao wa Matangi ni matokeo ya juhudi za pamoja zilizofanywa wakati wa Warsha ya Kwanza ya Wawasilianaji wa Mtandao wa Matangi, iliyofanyika tarehe 5 na 6 Novemba 2024, huko Brasília. Kwa sasa, mtandao huo unaundwa na wawakilishi kutoka maeneo ya mawasiliano ya Sekretarieti za Serikali za Majimbo zinazounda eneo la nusu-jangwa, pamoja na mashirika ya kiraia kutoka maeneo ya nusu-jangwa na Amazon, ambayo ni washirika wa Serikali ya Shirikisho katika utekelezaji wa Programu ya Matangi.

> **“Mtandao ni muundo wa mahusiano unaounganisha nodi au vituo vingi na vituo vingine vingi. Hii ni miunganisho kutoka sehemu nyingi kwenda sehemu nyingi, si kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingi.”**
>
> **Uelewa wa mazingira**





## FAHAMU ZAIDI

**Maji kwa ajili ya mustakabali: Miaka 20 ya Mpango wa Matangi** Wahariri: Camile Marques Sahb, Vitor Leal Santana, Márcia Muchagata. Brasília: Wizara ya Maendeleo na Misaada ya Kijamii, Familia na Kupambana na Njaa; Fiocruz; Zabelê Comunicação: 2024. Inapatikana katika: : https://www.gov.br/mds/pt-br/acoes-e-programas/acesso-a-alimentos-ea-agua/programa-cisternas

**Miongozo na machapisho mengine ya** kusaidia washirika katika usimamizi wa ugatuzi wa Mpango wa Matangi na kusaidia watafiti na wadau wengine kuelewa matokeo na athari za Mpango huu katika maisha ya walengwa wake. https://www.gov.br/mds/pt-br/acoes-e-programas/accesso-a-alimentos-ea-agua/programa-cisternas/manuais-e-outras-publicacoes

**Video kuhusu Mpango huu** https://www.youtube.com/results?search_query=%C3%A1gua+para+colher+futuro

**Utafiti na tathmini nyingine kuhusu Mpango huu** https://www.gov.br/mds/pt-br/acoes-e-programas/acesso-a-alimentos-ea-agua/programa-cisternas/resultados-e-avaliacoes

## MAWASILIANO


Wizara ya Maendeleo na Misaada ya Kijamii, Familia na Kupambana na Njaa – MDS

Sekretarieti ya Kitaifa ya Usalama wa Chakula na Lishe – SESAN

Idara ya Kukuza Masharti ya Uzalishaji Vijijini na Upatikanaji wa Maji – DFA

Uratibu Mkuu wa Upatikanaji wa Maji – CGAA

Esplanade ya Wizara, Ghorofa C, Chumba 442

Nambari ya posta: 70046-900 Brasilia/DF

Simu: +55 (61) 2030-1055

GLOBAL ALLIANCE
AGAINST HUNGER
AND POVERTY

WIZARA YA
MAENOELEONA MSAADA
WA KIJAMII,FAMILIA
NAKUPAMBANA NA NJAA

SERIKALI YA
BRASIL
UPANDE WA WATU WA BRAZILI